CASE FOR REFUGEES

centre for advocacy, support and education for refugees

Maelezo ya kuandaa Wosia

Wills - Swahili

Nini maana ya Wosia?

Wosia ni wakala ambao unaelezea ni kwa namna gani ungependa kugawa mali zako wakati utakapofariki. Mali zako zinaweza kuwa Ardhi, Fedha, Miliki na vitu vingine unavyovimiliki.

Wosia lazima ufanywe kwa hiari yako mwenyewe bila lazima kutoka kwa mtu mwingine.

Kwa nini unatakiwa kuandaa wosia?

Ni muhimu kuandaa wosia ili kuhakisha kwamba watu ambao umedhamilia kuwapa mali zako ndio hao hao watakopewa baada ya kifo chako.

Kama hauna wosia hautakuwa cha kusema jinsi gani mali zako zigawiwe kutokana na sheria za Austaria. Hii ina maana kuwa mali zako zitagawiwa kwa watu ambao hukupenda wapewe.

Pia wosia unakuruhusu kufanya mipango ya ulinzi/ulezi kwa kila mtoto na wengine wanaokutengemea , kupanga aina gani ya mazishi unayotaka na hata kama ungependa viungo vyako vitumike kusaidia watu wengine baada ya kifo chako.

Unatakiwa kuwa makini, ijapo kuwa wosia wako umepangwa kwa matakwa yako kipi kitakuwa cha muhimu zaidi. Ni haki kwa ndugu wa familia kukosoa wosia wako. Kwa mfano, Familia yako inaweza kukosoa ulinzi uliopanga kwa watoto wako au pendekezo lako lakuwa muhisani. Kwa sababu hii, ni muhimu sana kujadili na familia yako mapendekezo yako, kuhakikisha kuwa wanafuata yaliyomo katika wosia baada ya kifo chako.

Uhalali wa wosia

Kuhakikisha kuwa wosia wako ni halali lazima uwe na baadhi ya vigezo na uweke wazi kutoa vitu kwa baadhi ya ndugu wa familia. Kwa maelezo haya unatakiwa upate mwanasheria wa kukuchorea wosia wako. CASE Kwa wakimbizi inc. inaweza kukusaidai kuanda wosia kwa niaba yako.

Baadhi ya aina za rasilimali zako hazitatolewa kwa watu wengine kupitia wosia wako. Kwa mfano, kama unamiliki ardhi ambayo mmechangia na mtu mwingine basi baada ya kifo sehemu yako ya ardhi itabakiwa na mtu huyo bila kujalisha wosia wako uliotoa kwa mtu mwingine.

Wosia kuwa na uhalali lazima pia uwe kwa maandishi na kusainiwa na mashahindi halali. Kuna uhitaji maalumu kuhusu nani atakayekuwa shahidi wako.

Utatakiwa kumchangua msimamizi wa Mirathi ambaye atawajibika kuhakikisha kuwa mambo yote yaliyomo kwenye wosia yanatekelezwa. Kuna uhitaji maalumu kuhusu nani anaweza kuwa msimamizi wa mirathi.

Ni watu gani unatakiwa kuwagawia katika Wosia?

Sheria za Austaria zinaeleza kuwa kama baadhi ya watu hawakutosha katika wosia uliondaa, hapo wote hawatoruhusiwa kuomba baadhi ya mali au kuomba utoji wa vitu kwa akiba mbali na mali zako. Kwa mfano, watu ambao

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo tu wa ujumla na yasitumiwe badala ya Ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. Inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayomupata msomaji ikitokana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomaji lazima apate ushauri wa kisheria maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.

wanaweza kubishia wosia wako ni kama vile wake wa zamani na wasasa , wazazi , watoto na watu wengine ambao ni tegemezi kwako.

Kama hutataka kuacha mali yoyote kwa mtu yeyote ambaye alikuwa na haki ya kurithi mali yako kutokana na sheria za Australia, lazima utoe maelezo yako wazi katika wosia ukieleza lengo la kumtoa mhusika katika urithi wako. Hata kama ukifanya hivyo, hakuna uhakika kwamba mahakama itafuata mapendekezo yako . Hii ni sehemu ngumu katika sheria na unashauriwa kutafuta ushauri wa sheria kama unataka kumuondoa mmoja wapo katika wosia.

Wapi utahifadhi wosia wako?

Ni muhimu kuhifadhi wosia hasiri katika sehemu zenye ulinzi. Kwa mfano, unaweza kuchangua sehemu ya kuhifadhi wosia wako kwa mwanasheria, muhasibu, kwenye benki au sehemu yoyote unayoiamini.

Ni lazima utunze nakala ya wosia wako pamoja na maelezo ya sehemu gani wosia asili umehifadhiwa.

Hakikisha kuwa ambatanisha na kitu chochote katika wosia wako. Hii inaweza kuharibu ukweli wa wosia wako.

Wakati gani unatakiwa kurudia upya na kurekebisha wosia wako?

Kwa kawaida lazima ufikiri kuhusu kuangalia upya na kurekebisha wosia wako kila baada ya miaka miwili au mitatu.

Unatakiwa pia kubadilisha wosia wako wakati mazingira yako yanapobadilika, kwa mfano:

- Ndoa , Utengana na talaka au Mwanzo au Mwisho wa mahusiano yenu.
- Kuzaliwa au Kufa kwa ndugu katika Familia au
- Kufa kwa msimamizi wa Mirathi

Mabadiliko ya karibuni au ya sasa katika sheria yana maana kuwa kama utaoa au kuolewa baada ya kutengeneza wosia, ndoa yako italeta madhara ya utenguzi wa wosia wako, labda kama ndoa hiyo imo katika mkataba .Kama umepewa au kutoa talaka, wosia wako pia utatenguliwa.

Wapi pa kupata msaada?

CASE kwa wakimbizi inc. Sio taasisi ya kiserikali na sio ya kidini .Ambayo inasaidia wahamiaji na shughuli zote za kisheria.katika mila na isimu ya Lugha(Cald)katika jamii ya Australia magharibi. CASE kwa wakimbizi inc. inaweza kukusaidia kuandaa wosia kwa niaba yako.

Shughuli zote sio za malipo, ingawa misaada ya watu binafsi na mashirika tunaihitaji. Michango yote ya zaidi ya AUD $2.00 haina vati.

Kwa mawasiliano zaidi ya CASE kwa wakimbizi inc.ni haya yafuatayo :

145 Stirling Street, Perth
Western Australia 6000
Simu:(08) 92277311
Kinukushi: (08) 92277188

Email: admin@caseforrefugees.org.au

KANUSHO: Maelezo ya karatasi hii yanatoa mwongozo tu wa ujumla na yasitumiwe badala ya Ushauri wa kisheria. Kwa kiwango cha juu kinachoruhusiwa na sheria, CASE kwa wakimbizi Inc. Inakanusha hasara yoyote ya moja kwa moja au isiyo ya moja kwa moja itakayomupata msomaji ikitokana na kutegemea au kuhusiana na maelekezo katika karatasi hii. Msomaji lazima apate ushauri wa kisheria maalumu kutokana na mazingira ya mtu mwenyewe binafsi.